**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUTHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa natanguliza shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ambae ametujaalia uhai na taufiki ya kufika hapa tukiwa wazima na wenye afya njema. Namuomba tena Mwenyezi Mungu akuzidishie wewe Mheshimiwa Spika busara, hekma na uadilifu katika kutuongoza na sisi pia atujaalie tuendelee kuwa na nguvu na ari ya kuwawakilisha Wananchi na kusimamia vyema utekelezaji wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati ya PAC kuwa na jukumu la kuchambua na kutafakari ripoti ya ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali lakini pia inajukumu jengine la kujadili bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 107, Jadueli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo la Mwaka 2020).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu ilitekeleza jukumu hilo kwa kukutana na watendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali siku ya Jumatatu ya tarehe 26 Aprili, 2021 na kujadili pamoja na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa fedha 2021/2022.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati ya PAC imeridhika na utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2020/2021 pamoja na mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka 2021/2022 kama yalivyoainishwa katika Fungu E 04 la Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, kutokana na kasoro mbalimbai zilizobainika, Kamati yetu imetoa ushauri katika maeneo yanayohusika na kasoro hizo ili Bajeti ya Ofisi hii iweze kutekelezeka ipasavyo na kuleta tija inayokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kubainika kwa tofauti ya viwango vya fedha za Mapato na Matumizi ya Kawaida vilivyoainishwa katika Mswada wa Makadirio na zile vilivyoainishwa katika Hotuba ya Waziri husika, Kamati ya PAC ilishauri Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya marekebisho ya jumla ya fedha za Mapato na matumizi zilizoainishwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ili ziende sambamba na ile zilizoainishwa katika Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi.

**Mheshimiwa Spika, k**ama inavyofahamika kuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inategemea kupata mapato yake kupitia chanzo kimoja cha ada ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mashirika ya Serikali na Miradi ya Maendeleo ambapo kwa mwaka 2020/2021, Ofisi hii ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 225,000,000, Hadi kufikia mwezi Machi 2021 Ofisi hil imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 80,793,760.80 sawa na asilimia 36 ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika,** takwimu za Kamati ya PAC zinaonesha kuwa katika mwaka 2019/2020, Ofisi hii ya Mdhibiti awali ilikadiriwa na Wizara ya Fedha kukusanya Tsh 56,915,000 lakini Kamati ya PAC haikuridhika na Makadirio hayo na baada ya kufanya uchunguzi wake ilipendekeza makadirio mengine ya shilingi 158,000,000 ambayo yaliridhiwa na Wizara ya Fedha na kupitishwa na Baraza lako Tukufu. Hatimae, kwa mwaka huo wa fedha wa 2019/2020, Ofisi hii ya Mdhibiti iliweza kukusanya jumla ya shilingi. 98,306,233 kutokana na chanzo chake hicho cha mapato ya ada ya ukaguzi sawa na asilimia 62.2 ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka huu wa fedha wa 2021/2022, Ofisi hii ya Mdhibiti imekadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 283,012,000, ingawa Ofisi yenyewe kwa upande wake imedai kutokuwa na uwezo wa kufikia malengo ya kiwango hicho cha makusanyo.

**Mheshimiwa Spika**, ingawa hapa tunaizungumzia Bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini uzoefu wa Kamati ya PAC umebaini hali hii ya kutokuwepo kwa utaratibu wa uhakika wa upangaji wa makadirio katika Taasisi kadhaa za Serikali ambapo kuna baadhi ya Taasisi zikiwemo baadhi ya Idara Maalum za SMZ zimeonekana kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kukusanya na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kuliko zinavyokadiriwa.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na mazingira yote hayo, na ingawa Kamati ya Bajeti ina nafasi yake katika kulishughulikia suala hili, lakini ni dhahiri kuwa kuna haja kubwa kwa Wizara ya Nchi (AR) Fedha na Mipango kupitia Idara yake ya Masuala ya Kodi kuacha kukaa Ofisini muda mkubwa na badala yake kwenda wenyewe katika vyanzo vya

mapato na kufanya uchunguzi wa kina katika Taasisi zinazokadiriwa kukusanya mapato pamoja na kuwa karibu zaidi na Taasisi hizo ili kujua hali halisi ya vyanzo vya mapato katika Taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kufanya hivyo, kutapelekea kupanga makadirio yanayoakisi uhalisi wa vyanzo vya mapato vyenyewe na kuepusha kupanga makadirio madogo kwenye Taasisi zenye uwezo mkubwa wa kukusanya mapato pamoja na kuondoa malalamiko ya kupangiwa makadirio makubwa zaidi ya uwezo wa makusanyo kutoka katika Taasisi zinazokadiriwa. Aidha, hatua hii itaongeza mapato kwa Serikali ambayo kwa hivi sasa hayaingii katika Mfuko Mkuu.

**Mheshimiwa Spika**, kubwa zaidi, Kamati ya PAC imebaini changamoto ya kukosekana kwa uwezo wa Kisheria unaoipa Ofisi ya Mdhibiti uwezo wa kutoza ada ya Ukaguzi ingawa Ofisi hii imekuwa ikikadiriwa na kukusanya mapato hayo kwa kipindi kirefu sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Ukaguzi Namba 11 ya mwaka 2003 iiliyoweka masharti mbalimbali juu ya masuala ya Ukaguzi unaofanywa na Ofisi hii haikuipa Ofisi hii uwezo wa kuweka viwango au asilimia ya makusanyo kupitia kazi za Ukaguzi inazozifanya. Hali hiyo imepelekea baadhi ya Taasisi zinazotakiwa kulipa ada ya ukaguzi, kuhoji na kuiomba Ofisi ya Mdhibiti kutoa uthibitisho wa barua au wa kisheria unaoiruhusu Ofisi hii kudai ada au malipo yoyote baada ya kumaliza kazi za Ukaguzi katika Taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** hata ile ada ya asilimia kumi inayopatikana kutokana na ukaguzi unaofanywa kwa pamoja baina ya Ofisi hii na Taasisi nyengine za Ukaguzi (joint audit) nayo pia haina nguvu za kisheria bali yalikuwa ni maelekezo ya barua ya tarehe 21/3/2018 kutoka Wizara ya Fedha na Mipango iliyoitaka Ofisi hii kuzitoza asilimia hiyo kumi Taasisi zinazokagua kwa niaba yake.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile , kukosekana kwa nguvu za kisheria za Ofisi hii kukusanya mapato, kumeibua mwanya wa kukwepa kukaguliwa na kulipa ada ya ukaguzi kwa kuwa imebainika kuwa kuna baadhi ya Taasisi za Serikali ziilkuwa zikificha taarifa za kifedha (Financial Statement) za miradi yao ya Maendeleo kwa kuzichanganya taarifa za kifedha za miradi hiyo na taarifa za kifedha za Taasisi hizo ambapo kiutaratibu taarifa hizo za aina mbili hutakiwa kuandikwa mbali mbali. Kwa kawaida, Taasisi hutozwa ada ya ukaguzi baada ya taarifa hizo za miradi ya maendeleo kukaguliwa.

**Mheshimiwa Spika**, hayo yamefanyika bila hata ya Taasisi hizo kupewa adhabu yoyote kwa makosa hayo kutokana na kukoseknna kwa vifungu vya Sheria vinavyoweka masharti hayo,

**Mheshimiwa Spika,** utafiti uliofanywa na Kamati ya PAC umebaini kuwa zipo nchi nyingi ambazo ada zao za ukaguzi zimewekewa misingi imara ya kisheria na kuongeza ufanisi katika utendaji wa kazi wa Ofisi za Mdhibiti na Serikali zao kwa ujumla. Mifano ya vifungu mbalimbali vya Sheria za Ukaguzi katika nchi tofauti inathibitisha ukweli huu kama ifuatavyo:-

i. Kifungu cha 30 cha Sheria ya Ukaguzi Namba 7 ya mwaka 2008 ya nchi ya Uganda.
ii. Kifungu cha 41 cha Sheria ya Ukaguzi Namba 34 ya mwaka 2015 ya nchi ya Kenya.
iii. Kifungu cha 36 cha Sheria ya Ukaguzi Namba 25 ya mwaka 2004 ya Afrika ya Kusini kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2018.
iv. Kifungu cha 41 cha Sheria ya Ukaguzi Namba 11 ya mwaka 2008 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2020 pamoja na Kanuni za Ukaguzi za mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika**, hivyo ndivyo wenzetu walivyo, na kwa kuwa Zanzibar haiwezi kuachwa nyuma na kupitwa na mambo muhimu kama hayo, Kamati ya PAC inaisisitiza Wizara ya Nchi (AR), Katiba , Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuharakisha mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi namba 11 ya mwaka 2003 ili kuzirekebisha kasoro zote hizo ambapo rasimu ya marekebisho hayo ipo katika hatua ya Wizara kwa hivi sasa.

**Mheshimiwa Spika**, ni wazi kuwa marekebisho hayo ya Sheria ya Ukaguzi sio tu yataiongezea meno Ofisi hii, bali pia yataimarisha uwezo wake wa kukusanya na kuongeza mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, Kamati yetu imegundua kwamba yapo baadhi ya Mashirika ya Serikali yanakabiliwa na hali isiyoridhisha ya kifedha na yamekuwa hayaingizi chochote katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hali hiyo huathiri pia upatikanaji wa ada ya ukaguzi kwa kuwa Mashirika hayo huwa hayatozwi ada ya ukaguzi kutokana na hali yao ya kifedha. Ni matumaini ya Kamati yetu kuwa mkakati wa Serikali wa kuyafanyia uhakiki mashirika yote ya Serikali utazaa matunda ili mashirika hayo yaweze kutoa tija iliyokusudiwa kwa maslahi mapana ya nchi hii.

**Mheshimiwa Spika,** kama ilivyoelezwa hapo awali kuwa hadi kufikia mwezi Mach 2021, iOfisi ya Mdhibiti imeweza kukusanya jumla ya shilingi 80,793,760 sawa na aslimia 36 ya makadirio. Mapato hayo yanatokana na Taasisi na Miradi 16 iliyokaguliwa na kutozwa ada ya ukaguzi Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa yapo Mashirika

yameshakaguliwa lakini Ofisi ya Mdhibiti bado haijawasilisha ankara (invoice) za malipo. Katika Taasisi hizo. Hivyo, Kamati ya PAC inaishauri Ofisi hii kuwa ni vyema ikawasilisha ankara hizo katika Mashirika hayo ili yaweze kufanya malipo kwa matarajio kwamba itakapomaliza robo ya mwisho ya mwaka huu angalau mapato ya Ofisi ya Mdhibiti yaweze kufikia shilingi milioni 100,000,000.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, nadhani sote tunafahamu kuwa kazi za Ukaguzi ni kazi ngumu ambazo pamoja na kuhitaji sifa nyingi zikiwemo za uwajibikaji na uadilifu lakini pia zinahitaji utaalamu na weledi mkubwa ili kuweza kuzitekeleza kwa ufanisi unaotakiwa. Kwa msingi huo, Kamati imefarajika kuona kuwa katika utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Mwaka 2020/2021, pamoja kutekeleza kazi zake za Ukaguzi na kutoa Ripoti mbalimbali za Ukaguzi, Ofisi ya Mdhibiti imeweza kuwapatia mafunzo ya Ukaguzi yakinifu na ukaguzi wa kiuchunguzi wakaguzi 140 kati ya 156 waliopangiwa kupatiwa mafunzo, sawa na aslimia 89.74, pamoja na wafanya kazi wengine mbalimbali wanaopatiwa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka huu wa fedha wa 2020/2021, Ofisi hii inawasomesha wafanyakazi kumi na tatu (13) mafunzo ya muda mrefu katika fani tofauti zikiwemo za uhasibu na mafuta, Ni matumaini ya kamati kwamba watakapomaliza masomo wafanyakazi hao, wataisaidia Ofisi ya Mdhibiti kutanua wigo wa ukaguzi hata katika maeneo ya mafuta na gesi asilia.

**Mheshimiwa Spika,** kuongeza kasi ya kuwapeleka masomoni wafanyakazi wake ni suala la lazima kwa Ofisi hii kwani kuwekeza katika elimu, kutaisaidia Serikali na Ofisi hii kuweza kupata wafanyakazi wenye uwezo mkubwa zaidi wa kufanya ukaguzi katika maeneo yote ya Miradi ya Maendeleo na Mashirika hasa tukizingatia mwelekeo wa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kuuendeleza zaidi Uchumi wa Buluu pamoja na nyanja zinazoambatana nazo zikiwemo za mafuta na gesi.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, wakati Kamati yetu ilipokuwa ikipitia kwa undani makadirio ya matumizi ya Ofisi hii ilibaini kuwepo kwa kifungu kipya cha uratibu wa mipango, sera na utafiti (SE040203) ambacho hakikuoneshwa matumizi yake kwa mwaka uliopita, na kwa mwaka huu kuanza kupangiwa bajeti ya shilingi 315,872,000. Hivyo, Kamati inaomba Ofisi ya Mdhibiti kujipanga vizuri zaidi ili kufanikisha vyema malengo ya kuwekwa kwa kifungu hicho yakiwemo ya kuratibu na kusimamia masuala mbalimbali ya kisera, mipango na utafiti.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, sasa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala wa Bora, Katibu Mkuu, Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa

Hesabu za Serikali pamoja na watendaji wote wa Ofisi hiyo kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wa kupitia na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka huu wa fedha wa 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kuwashukuru Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii kwa moyo wao wa kujituma na mshikamano mkubwa waliouonesha na hatimae Kamati hii ikaweza kuipitia, kuichambua na kutoa mapendekezo yake kuhusu Bajeti ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima na taadhima, naomba niwatambue Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

1. Mhe, Juma Ali Khatib — Mweneyekiti;
2. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma — Makamo Mwenyekiti;
3. Mhe. Asha Abdalla Mussa — Mjumbe;
4. Mhe. Mihayo Juma N'hunga — Mjumbe;
5. Mhe. Yussuf Hassan Iddi — Mjumbe;
6. Mhe. Maryam Thani Juma — Mjumbe;
7. Mhe Sulubu Kidongo Amour — Mjumbe;
8. Ndg. Haji Khatib Haji — Katibu; na
9. Ndg. Said Khamis Ramadhan — Katibu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kwa mara nyengine kutamka kuwa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) imeyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2021/2022. naomba nichukue fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yano na hatimae waiuiunge mkono bajeti hii.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC), naunga mkono hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

……………………..

Juma Ali Khatib,

Mwenyekiti,

Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC),

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**